



MKOA WA KIGOMA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)



Simu Na. +255 028 2810339
Fax Na. +255 028 2810339
E-Mail/Baruapep:ded@kasuludc.go.tz
Website:www.kasuludc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
S. L. P 97,
Kasulu — Kigoma,
TANZANIA.

KUMB. NA. KSDC/S.2/6/VOL. IV/82

21 FEBRUARI, 2024

YAH: TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kwa mujibu wa **Kifungu cha 6 (1) (b)** cha Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 8 ya mwaka 2002 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2019 ikisomwa mintarafu na **Kifungu cha 111 (4) (a)** cha Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022 sura 298, anapenda kuwatangazia watanzania wenye sifa kuomba nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira ya Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu.

Masharti na Sifa za waombaji

- i/Awe Raia wa Tanzania.
- ii/Awe Mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu.
- iii/Awe Mstaafu katika Utumishi wa Umma.
- iv/Awe mwadilifu na uwezo wa kufanya kazi na kutoa maamuzi pasipo upendeleo.
- v/Awe na uwezo wa kuelewa Lugha ya Kiswahili na Kiingereza.
- vi/Awe na utambuzi katika masuala ya Utawala na Sheria.
- vii/ Awe na utambulisho kutoka kwa Mtendaji wa kijiji anachotokea.

Maombi yatumwe kwa posta, pia barua zinapokelewa Masijala ya Mkurugenzi Makao Makuu ya Halmashauri Nyakitonto. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **01 Machi 2024** saa 9.30 alasiri.
Barua zitumwe kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu,
S. L. P 97.
KASULU.

Joseph K. Rwiza,
MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA
KASULU.

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
KASULU
S. L. P. 97, KASULU